REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF ENVIRONMENT AND NATURAL RESOURCES
STATE DEPARTMENT OF ENVIRONMENT
KENYA METEOROLOGICAL DEPARTMENT
Dagoretti Corner, Ngong Road, P. O. Box 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya
Telephone: 254 (0) 20 3867880-7**, Fax:** 254 (0) 20 3876955/3877373/3867888,
e-mail: director@meteo.go.ke, info@meteo.go.ke
Website: http://www.meteo.go.ke

Ref. No. KMD/FCST/5-2017/SO/01-Kiswahili Date: 13th February 2017

TAARIFA YA MVUA YA MSIMU WA MACHI - APRILI - MEI 2017

MUKHTASARI
Utabiri wa Mvua ya Msimu wa Machi-Aprili-Mei (MAM) 2017

- *Mvua ya Msimu wa Machi-Aprili-Mei (MAM) 2017 inayojulikana kama "**Mvua ya Masika**" inatarajiwa kuwa pungufu mno. Sehemu zinazotarajiwa kuwa na mvua pungufu ni eneo lote la kaskazini na mashariki mwa nchi, maeneo yote ya pwani, tambarare za kusini mashariki mwa nchi na majimbo yote ya kati mwa nchi ikiwa ni pamoja na mji wa Nairobi.*

- *Nafuu kidogo itapatikana katika maeneo machache ya magharibi na kaskazini magharibi ambapo mvua inatarajiwa kuwa ya kiasi cha kawaida. Majimbo ya magharibi mwa nchi, kuna uwezokano wa kuwa na mvua yakutosha.*

- *Mgawo wa mvua utakuwa duni. Kutakuwa na vipindi virefu vya kiangazi ndani ya msimu.*

- *, sehemu nyingi vitaendelea na kiangazi mpaka karibu mwisho wa mwezi wa Machi.*

Lazima ifahamike kwamba mvua wakati huu inakuja wakati kuna ukame ulio sababishwa na mvua duni ya msimu uliopita. Ina maana kuwa sehemu zilizoadhirika itakuwa vigumu kupata nafuu kutokana na msimu wa masika unaotarajiwa kuwa duni pia.

*Tasmini hii ya msimu wa mvua ya Masika umefanywa kulingana na takwimu na taratibu za kisayansi, pamoja na vile hali ya joto inavyobadilika baharini. Ile hali ya **"La Nina"** katika Mashariki na Kati mwa Bahari ya Pasifiki bado ipo. Kila mara tunapopata hali hii ya **La Nina**, mvua za vuli na masika huku Afrika Mashariki huadhirika kiasi kikubwa.*

1. UTABIRI WA MVUA YA MSIMU WA MASIKA (MAM2017) KWA KINA

Msimu wa mvua ya masika (Machi-Aprili-Mei 2017) ni muhimu sana Kenya kwa sababu uzalishaji wa chakula, hasa mahindi huko maeneo ya Trans Nzoia na Uasin Gishu, hutumia mvua ya masika.

Utabiri kamili wa msimu wa mvua ya Masika ni kama ufuatavyo: (*Mchoro namba 1 chini)*

i. Mvua ya kawaida ya Msimu huu itapatikana;
Majimbo yalioko magharibi mwa nchi **(Busia, Bungoma, Vihiga, na Kakamega, Trans Nzoia, West Pokot na sehemu ya Turkana magharibi)**, na yale majimbo yanayopakana na Ziwa Victoria - majimbo ya Nyanza **(Kisumu, Siaya, Homa Bay, Nyamira, Migori, Kisii,..)**;

ii. Kati ya Kawaida na Chini ya kawaida;

Majimbo ya Kati mwa nchi **(Nyeri, Kiambu, Murang'a, Kirinyaga na Nyandarua, Meru, Embu na Tharaka**) na **jimbo la Nairobi;** majimbo yote ya mashariki mwa nchi; (**Makueni, Machakos, Kitui, Wajir, Isiolo, Garissa,Marsabit, Moyale**); majimbo ya Pwani (**Taita Taveta, Kwale, Mombasa, Tana River, Kilifi, Lamu**); na majimbo yalioko ndani ya Bonde la Ufa **(Samburu, West Pokot, Baringo, Laikipia, na Turkana**) na Majimbo ya Kaskazini Mashariki mwa Kenya (**Garissa, Wajir, Mandera**). Majibo mengine ni yale ya bonde la ufa kusini na kati; (**Kericho, Nandi, Bomet, Nakuru, Narok**);

2. MATARAJIO YA MGAWO WA MVUA YA MASIKA

Hali halisi ni kwamba mvua ya masika itakuwa chache na mgawo usio mzuri.

- Mwezi wa Machi ukame utaendelea sehemu nyingi isipokuwa maeneo ya magharibi ambapo mvua itakuwa imeanza wiki ya pili Machi.
- Mwezi wa Aprili mvua itakuwa imeanza kunyesha sehemu nyingi za mashariki mwa nchi na kufika kilele huko magharibi mwa nchi.
- Mwezi wa Mei mvua itaanza kukatika maeneo ya mashariki mwa nchi. Lakini magharibi mwa nci itaendelea hadi Juni.

3. MVUA YA MSIMU INATARAJIWA KUANZA NA KUMALIZIKA KAMA IFUATAVYO

	Majimbo	**Kuanza kwa Mvua**	**Kuisha kwa Mvua**
1	*Magharibi mwa nchi* ***(Busia, Bungoma, Vihiga, Kakamega, West Pokot, Trans Nzoia),*** *na majimbo ya* ***Nyanza (Kisumu, Siaya, Homa Bay, Nyamira, Migori, Kisii****)*	**Kati ya wiki ya pili na tatu Machi 2017**	**Mvua kuendelea mpaka Juni**
2	*Kusini mwa Bonde la ufa* ***(Narok na Kajiado)*** *Kati mwa nchi* ***(Nyeri, Kiambu, Murang'a, Kirinyaga na Nyandarua, Meru, Embu na Tharaka) na Nairobi***	**Kati ya wiki ya tatu na nne ya mwezi wa Machi 2017**	**Kati ya Wiki ya 3 hadi ya 4 Mei 2017**
3	*Kati mwa Bonde la Ufa* ***(Kericho, Nandi, Bomet, Uasin Gishu, Trans Nzoia, Nakuru, Narok);***	**Kati ya wiki ya tatu na nne ya mwezi wa Machi 2017**	**Mvua kuendelea mpaka Juni**
4	*Kusini mashariki mwa nchi* **Kitui, Makueni, Garissa, Tana River, Taita-Taveta na Kilifi**	**Kati ya Wiki ya tatu na nne Machi 2017**	**Kati ya Wiki ya pili na tatu Mei 2017**
5	*Pwani ya Kusini* **Kwale na Mombasa**	**Kati ya Wiki ya nne Machi na ya kwanza Aprili 2017**	**Kuendelea hadi Juni**
6	*Pwani ya Kaskazini* **Kilifi na Lamu**	**Kati ya Wiki ya kwanza na ya pili Aprili 2017**	**Kuendelea hadi Juni**

7	*Kaskazini Magharibi* **West Pokot, Samburu na Turkana**	**Kati ya wiki ya pili na ya tatu Machi 2017**	**Kati ya Wiki ya pili hadi ya tatu Mei 2017**
8	*Kaskazini Mashariki* **Isiolo, Marsabit, Wajir, Mandera na Garissa**	**Kati ya wiki ya kwanza hadi ya pili Aprili 2017**	**Kati ya Wiki ya pili hadi ya tatu Mei 2017**

4. VILE MVUA YA MSIMU (MACHI-APRILI-MEI 2017) ITAKAVYO ADHIRI SEKTA MBALIMBALI ZA UCHUMI

Uchumi wa Kenya unaegemea sana ukulima cha mvua. Kwa hiyo mvua inapokuwa pungufu uchumi nao huaadhirika vilivyo. Tasmini ya msimu huu inaonyesha sekta mbalimbali za uchumi zitaadhirika kiasi kikubwa: Kwa mfano;

4.1 **Sekta ya Kilimo, Chakula na Ufugaji**

1 Mvua pungufu inatarajiwa katika maeneo mengi ya kilimo nchini. Pia inatarajiwa, mvua itakuwa na mgawo ambao sio mzuri. Hali hii itaadhiri shughuli za kilimo katika maeneo mengi. Wakulima wanashauriwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ili wapewe ushauri wa matumizi bora ya mvua kwa kupanda mimea muwafaka, yanayostahimili ukame, hasa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua duni. Magharibi mwa Kenya, ambapo mvua inatarajiwa kuwa ya kutosha, vile vile wakulima wanapaswa kushirikiana na maafisa wa Wizara ya Kilimo ili wapewe ushauri jinsi ya kuongeza mazao.

2 Katika suala la uwepo wa chakula nchini, hali itakuwa ngumu kidogo. Kwa hiyo mikakati iliopo itabidi iendelee na wale walio na chakula cha akiba wanashauriwa wakihifadhi.

3 Hali ya malisho ya mifugo katika maeneo ya ufugaji kuna haja ya kutumia mbinu za kisasa (kama kununua bima) ili kuepuka hasara inayotokana na ukosefu wa lishe na maji.

4.2 Kitengo kinachokabiliana na Majanga (NDOC)

Kutokana na hali ya ukame inayokumba nchi yetu sasa hivi, hasa katika maeneo kame, maji na malisho ya mifugo yatakuwa ya shida. Kwa hiyo;

1. Kuna uwezekano wa kutokea mizozano kati ya jamii za ufugaji kutokana na malisho kidogo na uhaba wa maji katika maeneo ya huko Kaskazini magharibi na Kaskazini mashariki mwa Kenya.
2. Pia kuna uwezekano wa vita kati ya binadamu na wanyama wa porini juu ya uhaba wa maji katika maeneo ya mbuga za wanyama zilizoko maeneo kame. Mpango wa misaada ya vyakula na maji yapaswa kuendelezwa hata ikiwezekana kuongezwa ili kupunguza makali ya njaa katika maeneo kame.
3. Huko maghaibi mwa nchi - Kisii, Kisumu, Kakamega and Mt. Elgon radi huenda ikaadhiri sehemu hizo. Wenyeji wanaombwa wawe na tahadhari kubwa.
4. Mbali na kuwa mvua ni duni, kuna uwezekano wa mafuriko maeneo ya Budalang'i na Kano/Nyando. Pia kuna uwezekano wa maporomoko ya ardhi katika maeneo ya Murang'a, Nyeri na Elgeyo Marakwet.

4.3 Sekta ya Kawi na Uzalishaji wa Nishati

Kuna uwezekano wa kupata mvua ya kawaida katika maeneo ya vyanzio vya mito inayomimina maji yao Turkwel, Masinga na Sondu Miriu. Maji ya mabwawa yataongezeka na kuimarisha uzalishaji wa umeme.

4.4 Sekta ya Uchukuzi na Usalama Barabarani

Mbali na kuwa mvua ya msimu ni chache, kuna uwezekano wa kuwa na utelezi, ukungu, kupungua kwa upeo wa macho kutokana na dhoruba ya mvua nyingi na hata maporomoko. Ajali za barabara zinazohusishwa nah ii huenda zikatokea. Ni muhimu madereva wawe waangalifu sana.

4.5 Sekta ya maji

Kutokana na kiangazi kilichoko sasa, maji ya matumizi nyumbani na viwandani yatakuwa haba. Ni wajibu wa wahusika kugawa na kutumia maji yalioko kwa uangalifu mkubwa.

4.6 Sekta ya Afya ya Umma

Magonjwa yanayohusiana na uhaba wa maji na ukosefu wa mazingira safi kama vile homa ya matumbo na kipindupindu yanaweza kujitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi ambayo yanatarajiwa kupata mvua pungufu. Vile vile kutokana na kiangazi, magonjwa kama utapia mlo huenda yaadhiri watoto. Maafisa wa Wizara ya Afya ya Jamii wahusika wote wa Huduma za Kimatibabu wanashauriwa kuwa macho. Kuna haja ya kufanya mipango mapema kuwa na vifaa na madawa muhimu katika vituo vya afya ili kukabiliana na hali kama hizo zinapojitokeza. Kuna haja ya kugawa maji vizuri katika miji ili kuepuka maradhi.

4.7 Mazingira

Maeneo ambayo yanatarajiwa kuwa na mvua ya kutosha, wananchi wanahimizwa kutumia mbinu za kuzuia mmomonyoko wa udongo. Pia ni muhimu kuchukua fursa hii ya mvua na kuhifadhi mazingira kwa kupanda aina ya miti inayofaa.

5. **Ilani:**
    1. **Kumbuka:** utabiri huu lazima kutumiwa pamoja na utabiri unaotolewa kila siku, wiki hata mwezi na Idara hii.
    2. Utabiri wa kina wa kila jimbo utatolewa na maafisa wa Idara hii siku chache zijazo.

BW, PETER G. AMBENJE

MKURUGENZI WA HUDUMA ZA UTABIRI WA HALI YA HEWA NA MWAKILISHI WA KUDUMU WA KENYA KATIKA WMO



Mchoro Namba 1: Utabiri wa Mvua ya Msimu wa Machi-Aprili- Mei (MAM 2017)